

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA



Barua zote ziadikwe kwa:

Mkurugenzi mtendaji

Simu Na 0232402738,

Fax Na 023 2402706

Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P 10

MKURANGA

PWANI

Kumb.Na.LD/MK/6526

31/8/2020

Kamishna wa Ardhi Msaidizi,

Mkoa wa Pwani,

1 Mtaa wa Ardhi

S.L.P 9230,

Dar es salaam.

YAH: FOMU YA ARDHI NA. 1 YA KIWANJA NA. 53 KITALU 'E' VIKINDU
WILAYA YA MKURANGA


Rejea somo tajiwa hapo juu.

Tumepokea maombi ya Mwekezaji Kampuni ya **SRI BALAJI PHARMA LIMITED** wa **S. I. P. 40201 DAR ES SALAAM**. Kampuni hii inamilikiwa na wageni ambao ni RAMANJANEYA REDDY MUNNANGI SITA-INDIAN, VENU MADHAV PUTTA – INDIAN, SAMPATH KUMAR PUTTA – INDIAN, SANJAY RAMASHRAY SINGH – INDIAN, TARKESHWAR RAO KOLLATA – INDIAN, na VENU MADHAV PUTTA. Kampuni hii imenunua kiwanja namba 53 kitalu "E" eneo la Vikindu Wilaya ya Mkuranga,

Kampuni hii ya **SRI BALAJI PHARMA LIMITED** ilinunua kiwanja hiki kutoka kwa ndugu **ABUBAKAR SALUM RAJABU** wa **S. L. P. 22143 DAR ES SALAAM**, Kiwanja hiki hakikuwahi kuandaliwa hati.

Kiwanja hiki namba 53 Kitalu 'E' Vikindu kiliandaliwa kwa kufuata mchoro wa Mipango miji namba 19/VKD/02/012010 kwa matumizi ya **SERVICE INDUSTRY**

Halmashauri ya Wilaya imeandaa fomu ya Ardhi Na.1 na tunaiwasilisha kwako kwa hatua za maombi haya kujadiliwa na Kamati ya Ugawaji Ardhi Taifa na kisha kutangazwa kuwa eneo la uwekezaji kwa kuzingatia **Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 chini ya fungu la 19-20 sambamba Tangazo la Serikali Na.71 ya tarehe 4/5/2001 na Sheria ya Uwekezaji Na.26 ya mwaka 1997.**



Nawasilisha kwako taarifa za kiwanja tajwa nikiwa nimefungasha nyaraka zote za Kampuni iliyomba kumilikishwa Kiwanja hiki kwa ajili hatua zako stahiki.

Ngongi, menas,
Kny. Mkurugenzi Mtendaji (W)
Mkuranga

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P. 10,
MKURANGA.-Kwa taarifa

Sri Balaji Pharma Limited,
S. L. P. 40201,
DAR ES SALAAM- Kwa ufuatiliaji Wizarani